SOKOINE UNIVERSITY OF AGRICULTURE

OFFICE OF DEPUTY VICE CHANCELLOR
(ADMINISTRATION AND FINANCE)
P.O. BOX 3000, CHUO KIKUU, MOROGORO, TANZANIA
TELEPHONE:+255 023 2603511-4, Direct+255 023 2604653,
FAX: +255 0223 2604573
TELEGRAMS: UNIAGRIC – TELEX: 55308
E-mail: dvcadminfin@suanet.ac.tz

Our Ref No. SUA/ADM/P.1/4 **27/12/2011**

Wanajumuiya wote,

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo,

Morogoro.

YAH: TAARIFA KUHUSU MAAMUZI YA MKUTANO WA 122 WA BARAZA LA CHUO, ULIOFANYIKA KAMPASI KUU TAREHE 22 DESEMBA, 2011.

Baraza la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo "SUA Council" lilifanya mkutano wake wa kawaida wa 122 Kampasi Kuu ambapo lilipokea na kutolea maamuzi masuala mbalimbali ya shughuli za Chuo kama ifuatavyo:-

1. Baraza la Chuo lilipokea na kuridhia taarifa ya ushirikiano kati ya SUA na Chuo Kikuu cha Kwa Zulu Natal, Afrika ya Kusini kikishirikiana katika mkataba huo na Chuo Kikuu cha Malawi, na Chuo Kikuu cha Namibia. SUA na vyuo hivyo, vitashirikiana katika tafiti na uchambuzi wa masuala ya uhakika wa chakula na kutoa mafunzo yatakayohusu mbinu za uboreshaji wa upatikanaji chakula kulingana na mahitaji ya nchi zao.

2. Baraza lilipokea na kuridhia taarifa kwamba katika mwaka wa masomo wa 2011/2012, Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 1672 kwa mafunzo ya shahada za kwanza, stashahada na astashahada. Katika wadahiliwa hao, 1071 ni wanaume na 601 ni wanawake.

3. Baraza liliarifiwa na kuridhia taarifa kuwa wakati wa mahafali ya 27 ya " SUA", yaliyofanyika tarehe 25/11/2011, jumla ya wahitimu 1116 (wanaume 817 na wanawake 299) wa shahada za kwanza walitunukiwa shahada zao na Mkuu wa Chuo Mheshimiwa Al Noor Kassum.

4. Baraza liliarifiwa na kuridhia taarifa kuwa jumla ya wahitimu 195 wa shahada za Uzamili (wanaume 138, wanawake 57) na wahitimu wanane (8) wa shahada za uzamivu "PhD" (wanaume 6, wanawake 2) pia walitunukiwa shahada zao na Mkuu wa Chuo.

5. Aidha Baraza liliarifiwa na kuridhia kwamba jumla ya wahitimu 1,546 (wanaume 884, wanawake 662) walifuzu masomo mbalimbali ya astashahada, stashahada, shahada na stashahada za uzamili huko Chuo Kikuu cha Ushirika na Biashara "MUCCoBS" na kutunukiwa shahada zao wakati wa sherehe za mahafali zilizofanyika tarehe 2 Desemba, 2011.

6. Baraza la Chuo lilipokea na kuridhia mtaala mpya wa shahada ya uzamili inayoitwa "Master in Business Management" itakayoendeshwa "MUCCoBS" kuanzia mwaka wa masomo wa 2012/13.

7. Baraza la Chuo pia liliarifiwa na kuridhia kuwa mamlaka mbalimbali husika zimeridhia programu zifuatazo zianze kufundishwa "MUCCoBS" kuanzia mwaka wa masomo wa 2012/13:-
    (i) "Bachelor of Arts in Business Economics (BA – BEC)."
    (ii) "Bachelor of Science in Business Information and Communication Technology (BSc. BICT)."
    (iii) "Bachelor of Law (LLB)"
    (iv) "Master of Business Management (MBM)"

8. Baraza la Chuo lilipokea na kuridhia taarifa mbalimbali zifuatazo:-

(i) Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kurekebisha tarehe ya kumalizika kipindi cha sasa cha uongozi wa Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Balozi Nicholas A. Kuhanga cha miaka minne (4) kuwa Oktoba 31, mwaka 2012 badala ya tarehe 31 Oktoba, 2011 tangu alipoteuliwa tarehe Mosi Novemba 2008.

(ii) Mkuu wa Chuo Mheshimiwa Al Noor Kassum kumteua Profesa Gerald C. Monela kuwa Makamu wa Mkuu wa Chuo kwa kipindi kingine cha miaka mitano (5) kuanzia tarehe 6 Oktoba 2011 hadi tarehe 05 Oktoba, 2016.

(iii) Kufanyika kwa maadhimisho ya miaka 50 ya Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani USAID hapa SUA tarehe 27/10/2011 ambapo Mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mbunge), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wakati wa sherehe hiyo USAID ilikipatia Chuo ruzuku ya dola za kimarekani milioni moja.

(iv) Kufanyika kwa Mhadhara wa 12 wa Kumbukumbu ya Sokoine hapa chuoni tarehe 28/10/2011, uliotolewa na Mheshimiwa Cleopa David Msuya, Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(v) Kufanyika kwa Mjadala wa Kitaifa kuhusu miaka 50 ya Kilimo Tanzania Bara katika Kampasi ya Solomon Mahlangu tarehe 11 Novemba, 2011 ambao uliandaliwa na SUASA. Mgeni Rasmi alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mhe. Joel Nkaya Bendera ambaye alimwakilisha Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika Mhe. Prof. Jumanne A. Maghembe (Mbunge).

(vi) Kupokea wanafunzi wapya hapa chuoni kuanzia tarehe 24/10/2011 hadi 28/10/2011 na uzinduzi wa wiki hiyo ya uelimishaji wanafunzi wapya “Orientation Week”uliofanywa tarehe 25/10/2011 na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambaye aliwakilishwa na Mkurugenzi wa Elimu ya Juu Profesa Wilbard S. Abeli.

9. Baraza la Chuo lilitolea maamuzi masuala ya wafanyakazi mbalimbali kama ifuatavyo:-

    (i) Kukubali kuwapa wanataaluma wafuatao ajira ya mkataba wa miaka miwili:-

        (a) Profesa A.E. Pereka, Kitivo cha Tiba ya Mifugo
        (b) Profesa G.K. Mbassa, Kitivo cha Tiba ya Mifugo.
        (c) Profesa M.K. Kilasara, Kitivo cha Kilimo
        (d) Profesa J.J. Msaky, Kitivo cha Kilimo
        (e) Profesa K.P. Sibuga, Kitivo cha Kilimo
        (f) Dk. A. Luzi-Kihupi, Kitivo cha Kilimo

    (ii) Kukubali kuwaongezea wanataaluma wafuatao ajira ya mkataba wa miaka miwili:-

        (a) Profesa R.D. Mosha. Kitivo cha Tiba ya Mifugo
        (b) Profesa J.P. Mrema, Kitivo cha Kilimo
        (c) Profesa F.O.K. Mgongo, Kitivo cha Tiba ya Mifugo.

    (iii) Baraza liliagiza kuwa maombi ya kibali kwa ajira hizo yawasilishwe serikalini kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

K.A. Msagati

Kny: Naibu Makamu wa Mkuu wa Chuo (Utawala na Fedha).

Nakala:	Makamu wa Mkuu wa Chuo	) Ndani
”	Naibu Makamu wa Mkuu wa Chuo (Taaluma)	) ya
”	Naibu Makamu wa Mkuu wa Chuo (Utawala na Fedha)	) Jalada
”	Mbao za matangazo.	